
MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu




# Nafasi ya Kiswahili Katika Kupambana na Suala Ibuka la LGBTQ Mjini Mombasa

Patrick Jaika[a], Noah Majele[b*]

*Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo Kikuu cha Kaimosi, Kaimosi, Kenya*

*Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya*

**IKISIRI**

Tafiti tofauti kote ulimwenguni zimegundua mtu mmoja hadi kumi kati ya 100 wanavutiwa na wahusika wa jinsia moja. Moja ya dhihirisho la mapema zaidi ulimwenguni la ushoga ni michoro ya miamba ya watu wa San Zimbabwe ambayo inaonesha mahusiano ya jinsia moja ambalo ni suala la maelfu ya miaka iliyopita. Michoro hiyo ni ushahidi wa kihistoria unaonesha kuwa ushoga umekuwepo katika bara lote la Afrika katika historia yote na haujaletwa na mataifa ya Magharibi kama inavyodaiwa na viongozi wa kiafrika. Ijapokuwa, mwelekeo wa kimapenzi kwa kawaida hujadiliwa katika makundi matatu: mpenda jinsia tofauti kuwa na mvuto kwa wahusika wa jinsia nyingine, shoga ni mwanaume anayevutiwa na wanaume wengine ilhali msagaji ni mwanamke anayevutiwa na wanawake wenzake. Kwa mantiki hii makala haya yalichunguza nafasi ya Kiswahili katika kuliweka wazi suala ibuka la LGBTQ mjini Mombasa ambako watu hawazungumzii waziwazi. Makala haya yalitumia nadharia ya Ujenzi wa Jamii ambayo inaeleza kuwa katika mwingiliano wa jamii, maarifa na mitazamo huibuka kupitia mwingiliano wa watu. Vilevile nadharia hii hueleza jinsi dhana ya kijinsia inavyoundwa na kudumishwa katika jamii. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo na walengwa 200 walichaguliwa kimaksudi katika mji wa Mombasa. Hojaji ilitumiwa kupata data kutoka kwa walengwa hawa. Matokeo yalionesha kuwa Kiswahili kinachukuliwa kuwa chombo madhubuti cha kuhamasisha maadili ya kijamii, hasa kupitia vyombo vya habari, methali, semi, na elimu rasmi. Washiriki wengi walikubali kuwa Kiswahili kina uwezo wa kupinga tabia za LGBTQ kwa kufikisha ujumbe wa maadili na kuimarisha mshikamano wa kijamii. Hii ilionyesha kwamba Kiswahili kina nafasi muhimu katika kudumisha mitazamo ya kijinsia ya jadi na kupinga mabadiliko yanayohusiana na utambulisho wa kijinsia.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Mabasha,
Mashoga,
Pedofila,
Wasenge,
Wasagaji.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 27 Novemba 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 12 Machi 2026
Tarehe ya Kukubalika: 23 Machi 2026
Mtandaoni: 22 Aprili 2025

## 1. Utangulizi

Miaka ya hivi karibuni kumetokea kundi moja la vijana linalojulikana kama LGBTQ. LGBTQ ni kifupisho kinachotumika kuelezea kundi la watu wenye mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia usioendana na vigezo vya kijamii au kitamaduni vya kawaida. Kifupisho hiki kinajumuisha Lesbian (L), Gay (G), Bisexual (B), Transgender (T) na Queer (Q). Hata hivyo, mara nyingi, herufi ya "Q" inaweza kumaanisha pia "Questioning" ambapo watu wanaojiuliza kuhusu mwelekeo wao wa kijinsia au "Queer" ni neno la umbali unaozunguka mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia. Makundi haya yanapatikana katika miji mikuu nchini Kenya na kote duniani. Hata hivyo, utafiti huu ulinuia kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika katika kuhamasisha umma kuhusu kundi hili na athari zake katika jamii.

Utafiti huu ulifanyika mjini Mombasa kwa sababu mji huo unaaminika kuwa na watu wengi kwenye kundi hili (Oz na wenzake, 2023). Jones (2023) anaeleza kuwa kifupisho cha LGBTQ kinatokana na maneno ya Kiingereza, lakini kinatumika duniani kote na hata katika Kiswahili. Historia ya mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia ina mizizi ya kina, hata kama mara nyingi ilifichwa au kutengwa katika jamii nyingi za kihistoria. Kundi hili huwa halionekani wazi wazi kwa sababu za kuhofia kushambuliwa.

Katika tamaduni za kale, mwelekeo wa kijinsia ulikuwa umezingatiwa kwa njia tofauti. Kwa mfano, Green na wenzake (2022) wanaeleza kuwa, katika tamaduni za Kigiriki na Kirumi, uhusiano wa mapenzi kati ya wanaume ulikuwa sehemu ya utamaduni wa kijamii, hasa kati ya mwanaume mkubwa na mvulana mdogo katika muktadha wa pedofila au uhusiano wa kiuelekezi

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: nmajele@kibu.ac.ke

Mhariri: Leonard Chacha Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Nukuu: Jaika P. & Majele N. (2025). Nafasi ya Kiswahili Katika Kupambana na Suala Ibuka la LGBTQ Mjini Mombasa. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 31 – 39. https://doi.org/10.61889/kkcamc46.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

na mwanafunzi. Katika tamaduni za Kihindi, desturi kama "khawaja sara" (watu wa jinsia tatu) zilikuwa zikijulikana na kutambuliwa kama sehemu ya jamii (Green na wenzake, 2022). Hata hivyo, sehemu kubwa ya ulimwengu ina mwelekeo wa jinsia ulikuwa umeonewa au kutengwa, hasa wakati wa kuenea kwa dini na mabadiliko ya kijamii.

Lugha ya Kiswahili, kama lugha ya pili inayozungumzwa na watu wengi Afrika Mashariki na Kati, ina historia ndefu ya kutumika katika nyanja mbalimbali za maisha ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kama lugha ya mawasiliano, Kiswahili kimekuwa sehemu muhimu ya utambulisho wa jamii katika muktadha wa Afrika (Oz na wenzake, 2023). Hata hivyo, katika jamii nyingi za waswahili, kama ilivyo katika sehemu nyingi za dunia, jinsia imekuwa na nafasi muhimu katika miundo ya kijamii, utamaduni na masuala LGBTQ yamekuwa changamoto kubwa katika jamii hizi.

Robinson (2023) anaeleza kuwa jinsia moja inayohusisha uhusiano wa kimapenzi au kihisia kati ya watu wa jinsia moja, ni jambo ambalo limekuwa na upinzani mkubwa katika sehemu nyingi za dunia, na Afrika siyo tofauti. Katika jamii ya waswahili, masuala ya jinsia moja yamekuwa na changamoto nyingi, kuanzia mitazamo ya kijamii, utamaduni, hadi sheria na siasa. Hata hivyo, mabadiliko katika mtazamo wa kijamii, mabadiliko ya kisheria, na ushawishi wa harakati za kimataifa za haki za binadamu, umeanza kuleta mabadiliko jinsi jamii zinazozungumza Kiswahili zinavyoshughulikia masuala ya jinsia moja. Beasy na wenzake (2023) wanachangia kuwa nchini Tanzania, Kenya na Uganda asilimia ndogo ya watu wanasema kuwa serikali inapaswa kuhalalisha mapenzi ya jinsia moja. Asilimia kubwa wanakataa kuwa mapenzi na ndoa za jinsia moja ni haramu. Katika nchi zinazotumia Kiswahili, masuala ya jinsia moja yamekuwa ni yaliyopigwa marufuku kisheria. Nchini Kenya, Tanzania, Uganda, na nchi nyingine nyingi za Afrika Mashariki, ushirikiano wa kimapenzi kati ya watu wa jinsia moja ni kinyume cha sheria. Katika baadhi ya nchi hizi, kama vile Uganda, kuna sheria kali zinazohusiana na mapenzi ya jinsia moja huku baadhi ya sheria zikisababisha adhabu ya kifungo cha maisha au hata hukumu ya kifo kwa watu wanaoshiriki katika uhusiano wa jinsia moja.

Katika hali hii, Kiswahili kimekuwa sehemu ya mawasiliano ya kisiasa, ambapo serikali na viongozi wa dini hutumia lugha hiyo kuelezea msimamo wao dhidi ya mapenzi ya jinsia moja na kuunga mkono imani za kijamii na kidini dhidi ya mwelekeo wa LGBTQ. Hata hivyo, licha ya changamoto hizi, harakati za Kiswahili katika maeneo yenye LGBTQ zimekuwa zikikua na kutafuta mabadiliko ya kisheria na haki za msingi kwa ajili ya watu wa jinsia moja. Mfano ni pamoja na wanaharakati wa haki za kibinadamu kupigania haki na kubadilisha sheria kwa watu wa jinsia moja (Smith, 2022).

Makala hii iliangazia sehemu zifuatazo: uhakiki wa maandishi, misingi ya nadharia, mbinu za utafiiti na matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo na hitimisho. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza nafasi ya Kiswahili katika kupambana na suala ibuka la LGBTQ mjini Mombasa.

## 2. Uhakiki wa Maandishi

Lugha ya Kiswahili ni sehemu muhimu ya utambulisho wa jamii Afrika Mashariki, ikitumika katika nyanja za kisiasa, kijamii, na kitamaduni. Katika muktadha wa masuala ya LGBTQ, Kiswahili kinaweza kuwa chombo chenye nguvu ya kuimarisha maadili ya kijamii na kukabiliana na mitazamo inayohimiza tabia zinazokinzana na utamaduni wa Kiafrika. Badgett na wenzake (2021) wanasema kuwa lugha ina nguvu ya kushawishi mitazamo na tabia, hasa inapojikita katika maadili ya kijamii. Uhakiki huu unazingatia jinsi Kiswahili kinavyoweza kutumika kupinga LGBTQ kwa kufanikisha elimu ya maadili, kuimarisha mshikamano wa kijamii, na kuondoa unyanyapaa.

Kiswahili kinaweza kuwa chombo madhubuti cha kupinga LGBTQ kwa kutoa elimu inayohimiza maadili na mshikamano wa kijamii. Schreuder (2021) anaeleza kuwa lugha ya kiasili ni nyenzo muhimu ya kujenga nafasi za mawasiliano zinazosaidia jamii kuelewa masuala nyeti kama ya LGBTQ. Katika muktadha wa Kiswahili, methali na semi zinaweza kutumika kama njia ya kufundisha maadili yanayopingana na LGBTQ. Kwa mfano, methali zinazosisitiza heshima na mshikamano zinachangia kuimarisha maadili ya Kiafrika. Aidha, Mayo (2022) anaeleza kuwa elimu inayotumia lugha za kiasili husaidia jamii kuelewa changamoto za maadili na jinsi ya kuzitatua. Kwa kutumia Kiswahili, viongozi wa kijamii na kidini wanaweza kufanikisha kampeni za kuelimisha kuhusu hatari za LGBTQ katika jamii.

Methali, semi, na nyimbo za Kiswahili zina nafasi kubwa ya kufundisha maadili yanayokubalika kijamii. Haymer na wenzake (2020) wanaeleza kuwa methali na semi zimekuwa sehemu muhimu ya kufundisha vizazi mbalimbali kuhusu heshima na uadilifu. Semi kama "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu" zinaweza kufundisha vijana kuhusu athari za kupuuza maadili ya kijamii. Aidha, Paiz & Koda (2021) wanaonesha kuwa nyimbo za lugha ya kiasili zina nafasi ya kufanikisha kampeni za maadili. Kwa mfano, nyimbo zinazoimbwa kwa Kiswahili zinaweza kusisitiza umuhimu wa heshima na mshikamano wa kijamii, huku zikipinga mitazamo inayohimiza LGBTQ.

Vyombo vya habari ni njia bora ya kufanikisha kampeni dhidi ya LGBTQ kwa kutumia Kiswahili. Ro & Kang (2025) wanasema kuwa vyombo vya habari vinavyotumia lugha ya kiasili vina nafasi kubwa ya kufikia watu wengi na kuwashawishi kubadili mitazamo yao. Redio na televisheni zinazotumia Kiswahili zinaweza kuanzisha vipindi vya elimu vinavyoeleze hatari za LGBTQ na kuimarisha maadili. Wanaeleza kuwa matumizi ya lugha ya kiasili katika vyombo vya habari husaidia kupunguza unyanyapaa na kuimarisha mshikamano wa kijamii. Hii inadhihirisha kuwa Kiswahili

ni nyenzo madhubuti ya kufanikisha mawasiliano yanayolenga kupinga LGBTQ.

Ili kufanikisha kupinga LGBTQ, mikakati inayotumia Kiswahili inapaswa kujikita katika elimu, familia, na jamii. Ramsey na wenzake (2022) wanaonesha kuwa familia zina jukumu muhimu la kutumia lugha ya kiasili kufundisha maadili kwa watoto. Kwa mfano, wazazi wanaweza kutumia Kiswahili kueleza athari za tabia zisizokubalika kijamii na kuhimiza maadili yanayokubalika. Aidha, Chatterjee & Mukherjee (2020) wanasema kuwa semina na warsha zinazotumia lugha ya kiasili huimarisha uelewa wa vijana kuhusu changamoto za kijamii. Katika muktadha wa Kiswahili, warsha za vijana zinazohimiza mshikamano na maadili zinaweza kusaidia kupinga LGBTQ.

### 2.1. Maadili ya Kiafrika yanayokinzana na LGBTQ

Katika jamii nyingi za Kiafrika, uhusiano wa kijinsia unazingatiwa kuwa ni kati ya mwanaume na mwanamke pekee. Hii ni imani iliyozingatiwa katika tamaduni na desturi za kiafrika ambazo zimeimarishwa na mafundisho ya kidini na kisiasa. Uwepo wa jamii ya LGBTQ, ambayo inakubaliana na uhusiano wa jinsia moja, mara nyingi huonekana kuvuruga maadili haya ya kijinsia. Kaoma (2012) anasema kuwa, kuanzishwa kwa uhusiano wa jinsia moja katika muktadha wa Kiafrika kunaonekana kama jambo la kimagharibi linaloingia kwa nguvu na kinyume na tamaduni za Kiafrika, ambapo uhusiano wa kijinsia kati ya mwanaume na mwanamke ndio unaonekana kama njia pekee ya asili na kimaadili. Imani hii inadai kuwa uhusiano wa jinsia moja unahatarisha uadilifu wa jamii kwa kuwa ni dhana ya kigeni na isiyo ya asili.

Zaidi ya hayo, Okpokwasili (2024) anazungumzia athari za kimaadili ya ushoga katika jamii za Kiafrika, akisisitiza kuwa ushoga unachukuliwa kama ukiukaji wa maadili ya kijinsia ya jadi. Katika muktadha huu, jamii ya LGBTQ inachukuliwa kama kinyume na tamaduni za kijinsia zilizozingatiwa na jamii za Kiafrika, ambapo ndoa na uhusiano wa kijinsia unategemea uhusiano wa mwanaume na mwanamke. Hii ni kwa sababu ndoa ya jinsia tofauti inatambulika kama msingi wa kudumisha utaratibu wa kijamii na umoja, hivyo, upinzani dhidi ya LGBTQ ni mkubwa katika jamii nyingi za Kiafrika.

Familia ni kitengo cha msingi katika jamii nyingi za Kiafrika, ambapo ndoa kati ya mwanaume na mwanamke inatambulika kama msingi wa familia na urithi. Katika tamaduni za Kiafrika, familia inadhihirika si tu kama taasisi binafsi, bali pia ni ishara ya uthabiti na umoja wa kijamii. Saheed (2023) anasema kuwa familia inatambulika kuwa ni sehemu muhimu ya utamaduni na ustawi wa kijamii, ambapo ndoa kati ya mwanaume na mwanamke ina maana ya kuzaa watoto na kuendeleza urithi wa familia. Kwa hivyo, uhusiano wa jinsia moja unapingana na msingi huu wa familia, kwani hauleti watoto kupitia uzazi wa asili.

Aidha, Mbaru na wenzake (2018) wanasisitiza kuwa utambuzi wa haki za LGBTQ katika jamii za Kiafrika unakutana na upinzani mkali, kwani uhusiano wa jinsia moja haukidhi kazi ya familia katika tamaduni za Kiafrika, ambayo ni kuzaa watoto na kudumisha uhusiano wa kijamii. Hivyo, jamii za Kiafrika mara nyingi kuona mapenzi ya jinsia moja kama kitisho kwa muundo wa familia wa jadi, kwani hayawezi kuchangia katika kuendeleza urithi wa familia au jamii kwa njia ya kijinsia.

Katika jamii za Kiafrika, majukumu ya kijinsia yamejulikana wazi ambapo wanaume wanatarajiwa kuwa watoa riziki na waangalizi ilhali wanawake wanatarajiwa kuwa na wajibu wa huduma za nyumbani na familia. Mthembu (2023) anasema kuwa jamii nyingi za Kiafrika zina imani thabiti kwamba majukumu haya ya kijinsia ni muhimu kwa uthabiti wa kijamii na kimaadili. Vilevile, viongozi wa kitamaduni na kidini wanathamini na kudumisha mgawanyo huu wa kijinsia. Hata hivyo, uwepo wa jamii ya LGBTQ, ambayo inahusisha uhusiano wa jinsia moja na utambulisho wa kijinsia usio wa kike wala wa kiume, unapingana na mgawanyo huu wa kijinsia.

Kwa upande mwingine, Ugwu na wenzake (2025) wanajadili jinsi majukumu ya kijinsia katika jamii za Kiafrika yamejikita katika tamaduni na desturi zinazojumuisha mifumo ya kijinsia ya kiume na kike. Kukubalika kwa utambulisho wa jinsia nyingine na mahusiano ya jinsia moja kunapingana na mfumo huu wa kijinsia na kuleta upinzani mkubwa. Hii inamaanisha kuwa, jamii nyingi za Kiafrika, mapinduzi katika mifumo ya kijinsia ni tishio kwa utulivu na usalama wa kijamii na kuleta hali ya kutokuwa na uhakika kuhusu mustakabali wa jamii.

## 3. Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ujenzi wa Jamii iliyoanzishwa na Butler (1990) na kuendelezwa na Seartle (1995). Nadharia hii inasisitiza kuwa mwingiliano wa kijamii, maarifa, na mitazamo hutokana na mwingiliano kati ya watu. Kwa msingi wa nadharia hii, maarifa ya jamii huundwa kupitia makubaliano ya kijamii yanayojitokeza katika mazingira ya kijamii na kupitia matumizi ya lugha kama chombo muhimu cha kuwasilisha na kujenga maana.

Nadharia ya Ujenzi wa Jamii ina mihimili kadhaa muhimu. Kwanza, ukweli ni wa kijamii, ikimaanisha kuwa maarifa, dhana, na uelewa wa mambo kama jinsia, utamaduni, au tabia za mtu hupatikana kupitia makubaliano ya kijamii. Pili, lugha huchukua nafasi muhimu kama chombo cha msingi cha kujenga na kuwasilisha maana. Kupitia lugha, watu hujenga "ukweli" ambao mara nyingi hutegemea muktadha wa kijamii. Aidha, mazingira ya kijamii yanahusiana na jinsi watu wanavyoathiriwa na hali ya kijamii na kitamaduni inayowazunguka, ambayo huchangia jinsi wanavyotafsiri

na kuelewa ulimwengu wao. Hatimaye, mwingiliano wa kijamii ni mhimili mwingine muhimu, ambapo maarifa na mitazamo huibuka kupitia mazungumzo na ushirikiano wa kijamii.

Utafiti huu ulizingatia mihimili mitatu ya Nadharia ya Ujenzi wa Jamii: Ukweli kama kijamii, mazingira ya kijamii na mwingiliano wa kijamii. Mihimili hii ilitumika kueleza jinsi maarifa na mitazamo inavyotokana na mwingiliano wa watu katika muktadha wa kijamii na kitamaduni. Nadharia hi ilifaa kwa utafiti huu kwa sababu iliweza kueleza ukweli wa jamii, mazingira ya kijamaii na mwingiliano wa kijamii.

## 4. Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu uliwezesha kuchunguza jinsi Kiswahili kilivyotumika katika kuimarisha maadili ya kijamii na kupinga tabia zinazohusiana na LGBTQ. Muundo wa kimaelezo ulifaa kwa sababu ulilenga kupata maoni ya washiriki kuhusu mitazamo yao na uzoefu wao wa kijamii. Utafiti ulifanyika mjini Mombasa, Kenya. Mombasa ilichaguliwa kwa sababu ni mji wenye mchanganyiko mkubwa wa kitamaduni na kijamii, ambapo Kiswahili kinatumika kwa kiwango kikubwa. Aidha, mji huu ulionekana kuwa na uwakilishi mzuri wa mitazamo mbalimbali kuhusu LGBTQ. Utafiti ulilenga washiriki 200 kutoka makundi mbalimbali ya kijamii mjini Mombasa, ukizingatia vigeu kama umri (chini ya miaka 18, 18-25, 26-35), kiwango cha elimu (shule ya msingi, sekondari, chuo, hakuna elimu rasmi), na utambulisho wa jinsia (wanaume, wanawake, na wengine kutoka jamii ya LGBTQ). Mbinu ya sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuchagua washiriki wa utafiti. Sampuli hii ilihakikisha kuwa walengwa waliwakilisha makundi mbalimbali ya kijamii na walikuwa na ufahamu kuhusu nafasi ya Kiswahili katika kupinga LGBTQ. Data zilikusanywa kwa kutumia hojaji. Hojaji zilikuwa na maswali yaliyolenga kupata maoni ya washiriki kuhusu nafasi ya Kiswahili katika kushughulikia masuala ya LGBTQ. Data ilichambuliwa kwa kutumia takwimu za kimsingi kama asilimia, na matokeo yaliwasilishwa kupitia jedwali na grafu

## 5. Matokeo na mjadala

Sehemu hii inachunguza matokeo ya utafiti na kuyajadili kwa kuzingatia muktadha wa kijamii na nadharia husika. Inajumuisha uelewa wa washiriki kuhusu LGBTQ, jukumu la Kiswahili katika kupinga tabia hizi, na maoni ya kijamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kama chombo cha maadili. Aidha, mjadala huu unatoa mapendekezo yanayolenga kutumia Kiswahili kwa njia bunifu ili kuimarisha mshikamano wa kijamii na maadili ya Kiafrika, huku ukipendekeza mbinu za kupunguza unyanyapaa na dhana potofu dhidi ya LGBTQ.

### 5.1. Habari za kimsingi

Walipoulizwa kuhusu jinsia yao, washiriki walionesha utofauti mkubwa: 40 walijitambulisha kama wanaume, 20 kama wanawake, na 140 kama jinsia nyingine, wakiwemo wasagaji, mabasha, wasenge, na mashoga. Idadi kubwa ya "jinsia nyingine" inaonesha uwepo wa kundi kubwa la LGBTQ mjini Mombasa, ikionesha mabadiliko ya kijamii na kuibuka kwa utambulisho wa kijinsia usio wa jadi, licha ya changamoto za unyanyapaa katika jamii.

Walipoulizwa kuhusu umri wao, washiriki waligawanyika katika makundi yafuatayo: 70 walikuwa chini ya miaka 18, 120 walikuwa na umri wa kati ya miaka 18-25, na 10 walikuwa na umri wa miaka 26-35. Takwimu hizi zinaonesha kuwa kundi kubwa zaidi la washiriki lilikuwa vijana wa umri wa miaka 18-25, ikifuatiwa na wale walio chini ya miaka 18, jambo linaloonesha uwakilishi mkubwa wa vijana katika utafiti huu.

Walipoulizwa kuhusu kiwango chao cha elimu, washiriki walionesha mchanganuo ufuatao: 61 walikuwa na elimu ya shule ya msingi, 130 walikuwa na elimu ya shule ya sekondari, 7 walikuwa na elimu ya chuo au elimu ya juu, na 2 hawakuwa na elimu rasmi. Takwimu hizi zinaonesha kuwa idadi kubwa ya washiriki walikuwa na elimu ya sekondari, ikifuatiwa na wale wa elimu ya msingi, huku walio na elimu ya juu na wasio na elimu rasmi wakiwa wachache.

### 5.2. Uelewa wa LGBTQ

Sehemu hii inachunguza kiwango cha uelewa wa washiriki kuhusu LGBTQ, ikionesha dhana zinazofahamika zaidi kama ushoga na usagaji, huku zingine kama mabasha na masenge zikieleweka kwa kiwango kidogo. Utafiti unaonesha kuwa kuna haja ya kuelimisha zaidi jamii kuhusu masuala haya ili kupunguza dhana potofu na unyanyapaa. Walipoulizwa kuhusu uelewa wao wa LGBTQ, washiriki walionesha yafuatayo: 63 walielewa kuhusu ushoga, 44 kuhusu usagaji, 39 kuhusu ubadilishaji wa jinsia (masenge), 36 kuhusu utambulisho wa kijinsia tofauti (mabasha), na 18 hawakuwa na uhakika. Takwimu hizi zinaonesha kuwa ushoga ulikuwa dhana inayofahamika zaidi miongoni mwa washiriki, huku kiwango cha kutokuwa na uhakika kikiwa cha chini zaidi. Jed. 1 linaonesha Uelewa wa Washiriki Kuhusu LGBTQ.

Jed. 1: Uelewa wa Washiriki Kuhusu LGBTQ

| Dhana ya LGBTQ | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ushoga | 63 | 31.5 |
| Usagaji | 44 | 22.0 |
| Ubadilishaji wa jinsia (Masenge) | 39 | 19.5 |
| Utambulisho wa kijinsia tofauti (Mabasha) | 36 | 18.0 |
| Sina uhakika | 18 | 9.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa 31.5% ya washiriki walikuwa na uelewa wa ushoga, dhana inayofahamika zaidi, ikifuatwa na usagaji kwa 22%. Uelewa wa ubadilishaji wa jinsia (19.5%) na utambulisho wa kijinsia tofauti (18%) ulikuwa chini, huku 9% ya washiriki wakibainisha kuwa hawakuwa na uhakika kuhusu LGBTQ.

Hii inaonesha kuwa ingawa baadhi ya dhana za LGBTQ zinafahamika vyema, zingine bado hazijulikani au hazieleweki kikamilifu miongoni mwa washiriki.

Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Shaikh na wenzake (2024), ambao ulibaini kuwa dhana za ushoga na usagaji zinafahamika zaidi katika jamii nyingi, hasa mijini. Aidha, uelewa wa masuala ya LGBTQ mara nyingi unategemea mijadala ya wazi na upatikanaji wa taarifa sahihi, jambo linalokosekana katika jamii nyingi za Afrika Mashariki. Matokeo haya yanasisitiza umuhimu wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kuelimisha ili kuimarisha uelewa wa masuala ya LGBTQ na kupunguza unyanyapaa unaotokana na dhana potofu. Walipoulizwa kama wanaamini kuwa tabia za LGBTQ zimeenea miongoni mwa vijana mjini Mombasa, washiriki walitoa majibu yafuatayo katika Jed. 2.

**Jed. 2**: Imani kuhusu Ueneaji wa Tabia za LGBTQ Miongoni mwa Vijana

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 153 | 76.5 |
| Hapana | 37 | 18.5 |
| Sina uhakika | 10 | 5.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa 76.5% ya washiriki wanaamini kuwa tabia za LGBTQ zimeenea miongoni mwa vijana mjini Mombasa. Hii inaashiria mtazamo mkubwa wa kijamii kuhusu ongezeko la tabia hizi. Kwa upande mwingine, 18.5% hawakubaliani na kauli hii, huku 5% wakiwa hawana uhakika. Uwiano huu unaonesha kuwa kuna utambuzi mkubwa wa uwepo wa LGBTQ miongoni mwa vijana, ingawa kuna baadhi ya watu wanaokosa maarifa au wanapinga wazo hilo.

Matokeo haya yanaonesha kuwa, makundi ya LGBTQ yanaonekana zaidi kutokana na mwingiliano wa kijamii na urahisi wa kuunda jumuiya. Hali kama hii inathibitishwa na Oakenfull (2024), inayobainisha kuwa mijini, watu wanaweza kufahamika kwa urahisi kama sehemu ya LGBTQ, hasa katika maeneo yenye mtazamo wa kidemokrasia zaidi. Matokeo haya yanasisitiza umuhimu wa kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya LGBTQ kwa lengo la kuondoa unyanyapaa na dhana potofu miongoni mwa vijana na wakazi wa mijini.

### 5.3. Jukumu la Kiswahili katika kupambana na LGBTQ

Sehemu hii ilitafiti jinsi Kiswahili kinavyoweza kutumika kama chombo cha kupinga LGBTQ. Washiriki wengi wanaamini kuwa Kiswahili kinaweza kufikisha ujumbe wa maadili kwa ufanisi kupitia vyombo vya habari, methali, semi, na elimu rasmi, likiwa chombo cha kuimarisha mshikamano wa kijamii. Kiswahili kinapinga LGBTQ kwa kuwa kinatumika kama chombo cha kudumisha maadili ya kijamii na tamaduni za Kiafrika, ambazo zinazingatia ndoa na uhusiano wa jinsia tofauti. Methali, semi, na vyombo vya habari vya Kiswahili vina nguvu ya kufundisha maadili ya kijinsia ya jadi, kuimarisha mshikamano wa kijamii, na kupinga mabadiliko yanayotokea katika masuala ya familia na jinsia. Kiswahili kinatumika kutoa elimu kuhusu umuhimu wa familia ya kiume na kike na kuunga mkono mtazamo wa kijamii dhidi ya LGBTQ, ili kudumisha misingi ya kijinsia ya jadi. Walipoulizwa kama lugha ya Kiswahili inaweza kusaidia kupinga tabia za LGBTQ, washiriki walitoa majibu yafuatayo: Ndiyo (169), Hapana (20), na Sina uhakika (11). Kama ilivyo kwenye Jed. 3.

**Jed. 3**: Uwezo wa Kiswahili Kupinga Tabia za LGBTQ

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 169 | 84.5 |
| Hapana | 20 | 10.0 |
| Sina uhakika | 11 | 5.5 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa idadi kubwa ya washiriki (84.5%) wanaamini kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kupinga tabia za LGBTQ. Washiriki hawa wanatambua nafasi ya Kiswahili kama lugha inayoweza kufikisha ujumbe wa maadili na kushawishi mtazamo wa kijamii. Kwa upande mwingine, 10% ya washiriki walikataa wazo hili, huku 5.5% wakisema hawana uhakika, jambo linaloweza kuonesha kutokubaliana kwa baadhi ya watu kuhusu ufanisi wa Kiswahili katika masuala haya.

Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Oakenfull (2024), ambao ulionesha kuwa lugha za asili zina nguvu ya kushawishi mitazamo na maadili ya kijamii. Aidha, Rojo (2022) katika nadharia ya Ujenzi wa Jamii, anaeleza kuwa lugha ni chombo cha msingi cha kuunda na kuimarisha ukweli wa kijamii. Matokeo haya yanaonesha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika si tu kama lugha ya mawasiliano, bali pia kama chombo cha kuimarisha maadili na kupunguza unyanyapaa unaohusiana na LGBTQ. Walipoulizwa kama Kiswahili kinatumika ipasavyo kufundisha maadili na utamaduni wa Kiafrika, washiriki walitoa majibu yafuatayo: Ndiyo (140), Hapana (50), na Sina uhakika (10). Kama ilivyo kwenye Jed. 4.

**Jed. 4**: Mtazamo Kuhusu Matumizi ya Kiswahili Kufundisha Maadili na Utamaduni wa Kiafrika.

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 140 | 70.0 |
| Hapana | 50 | 25.0 |
| Sina uhakika | 10 | 5.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya washiriki (70%) wanaamini kuwa Kiswahili kinatumika ipasavyo kufundisha maadili na utamaduni wa Kiafrika. Washiriki hawa wanatambua kuwa Kiswahili ni lugha yenye mizizi ya kitamaduni na uwezo wa kufikisha mafunzo ya maadili. Hata hivyo, 25% ya washiriki hawakubaliani na mtazamo huu, na 5% hawakuwa na uhakika, jambo linaloweza kuonesha kuwa bado kuna changamoto katika matumizi ya Kiswahili kama chombo cha kuimarisha maadili katika baadhi ya jamii.

Matokeo haya yanathibitisha kuwa lugha za kiasili kama Kiswahili zina jukumu muhimu katika kudumisha tamaduni na kuimarisha mshikamano wa kijamii (Li & Fabbre, 2022). Aidha, nadharia ya Ujenzi wa Jamii wanaeleza kuwa lugha ni msingi wa kujenga mitazamo ya kijamii, hasa kupitia mazungumzo na elimu. Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kuendeleza Kiswahili kama lugha ya kufundishia ili kudumisha maadili na utamaduni wa Kiafrika. Walipoulizwa kama methali na semi za Kiswahili zina nafasi ya kuimarisha maadili dhidi ya LGBTQ, washiriki walitoa majibu yafuatayo: Ndiyo (145), Hapana (30), na Sina uhakika (25). Kama ilivyo kwenye Jed. 5.

**Jed. 5**: Mtazamo kuhusu Nafasi ya Methali na Semi za Kiswahili katika Kuimarisha Maadili Dhidi ya LGBTQ.

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndio | 145 | 72.5 |
| Hapana | 30 | 15.0 |
| Sina uhakika | 25 | 12.5 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya washiriki (72.5%) wanaamini kuwa methali na semi za Kiswahili zinaweza kusaidia kuimarisha maadili dhidi ya LGBTQ. Hii inaonesha imani ya washiriki katika nguvu ya methali na semi kama njia ya kufundisha na kuimarisha maadili ya kijamii. Hata hivyo, 15% ya washiriki hawakubaliani na wazo hili, na 12.5% hawakuwa na uhakika, jambo linaloweza kuonesha changamoto za kufanikisha matumizi ya methali na semi katika muktadha wa kisasa. Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Villarroya & Boté-Vericad (2023) waliobainisha kuwa dhana za maadili zinahitaji kuunganishwa na mifumo ya kitamaduni ili kuongeza ushawishi. Matokeo haya yanasisitiza umuhimu wa kurudisha nafasi ya methali na semi za Kiswahili katika mazungumzo ya kijamii ili kuimarisha mshikamano wa kijamii na maadili.

### 5.4. Maoni ya Kijamii kuhusu Kiswahili na LGBTQ

Sehemu hii inaangazia mitazamo ya jamii kuhusu jinsi Kiswahili kinavyotumika katika kuhamasisha maadili. Inaonesha kuwa vyombo vya habari na viongozi wa kidini wanatumia Kiswahili kwa kiwango kikubwa, lakini changamoto bado zipo katika kufikia sehemu zote za jamii.

Walipoulizwa kama vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili vinahamasisha vijana kushikamana na maadili, washiriki walitoa majibu yafuatayo: Ndiyo (150), Hapana (31), na Sina uhakika (19). Kama ilivyo kwenye Jed. 6. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya washiriki (75.0%) wanaamini kuwa vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili vinahamasisha vijana kushikamana na maadili. Hii inadhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha yenye nguvu katika kufanikisha mawasiliano yenye athari chanya kwa vijana. Hata hivyo, 15.5% ya washiriki walikataa wazo hili, huku 9.5% wakiwa hawana uhakika. Hii inaashiria kuwa licha ya nguvu ya vyombo vya habari vya Kiswahili, changamoto bado zipo katika ufanisi wa ujumbe wao.

**Jed. 6**: Mtazamo kuhusu Vyombo vya Habari Vinavyotumia Kiswahili na Uhamasishaji wa Maadili.

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 150 | 75.0 |
| Hapana | 31 | 15.5 |
| Sina uhakika | 19 | 9.5 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Westwood (2022) ambao ulionesha kuwa vyombo vya habari vina jukumu muhimu katika kuimarisha maadili ya kijamii, hasa kupitia matumizi ya lugha za asili kama Kiswahili. Aidha, vyombo vya habari ni njia bora ya kufundisha na kuimarisha mitazamo ya kijamii, hasa miongoni mwa vijana. Hii inaonesha kuwa Kiswahili kinabaki kuwa chombo chenye ushawishi mkubwa katika kujenga mshikamano wa kijamii na kuimarisha maadili. Walipoulizwa kama viongozi wa kijamii na kidini wanatumia Kiswahili kufikisha ujumbe wa maadili, washiriki walitoa majibu yafuatayo: Ndiyo (160), Hapana (30), na Sina uhakika (10). Kama ilivyo kwenye Jed. 7.

**Jed. 7**: Mtazamo kuhusu Matumizi ya Kiswahili na Viongozi wa Kijamii na Kidini katika Kufikisha Maadili.

| Jibu | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 160 | 80.0 |
| Hapana | 30 | 15.0 |
| Sina uhakika | 10 | 5.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 80 ya washiriki wanaamini kuwa viongozi wa kijamii na kidini wanatumia Kiswahili kwa ufanisi kufikisha ujumbe wa maadili. Hii inaonesha nafasi muhimu ya viongozi hawa katika kutumia Kiswahili kama lugha ya kuunganisha jamii na kuimarisha maadili. Hata hivyo, 15% ya washiriki walikataa wazo hili, na 5% walikuwa hawana uhakika, jambo linaloweza kuonesha kuwa baadhi ya jamii zinakosa kushirikishwa ipasavyo.

**Jed. 8**: Mapendekezo ya Njia za Kutumia Kiswahili Kupinga LGBTQ.

| Njia | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Programu za redio na televisheni | 80 | 40.0 |
| Vitabu/nyimbo za Kiswahili | 50 | 25.0 |
| Semina na warsha | 40 | 20.0 |
| Methali mpya | 30 | 15.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Matokeo haya yanathibitisha Nadharia ya Ujenzi wa Jamii, ambayo inaonesha kuwa viongozi wa kijamii na kidini wanashiriki jukumu muhimu katika kujenga mitazamo na maadili ya kijamii kupitia lugha. Wilkins na wenzake (2022) walionesha kuwa matumizi ya lugha za asili kama Kiswahili yanaongeza ushawishi wa ujumbe wa maadili. Matokeo haya yanasisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi za viongozi hawa ili kuhakikisha ujumbe wa maadili unafikia sehemu kubwa ya jamii kwa lugha inayoeleweka na kukubalika.

### 5.5. Mapendekezo kuhusu matumizi ya Kiswahili dhidi ya LGDBTQ

Sehemu hii inatoa mapendekezo kutoka kwa washiriki kuhusu njia bora za kutumia Kiswahili kupinga LGBTQ. Mapendekezo yanajumuisha programu za vyombo vya habari, matumizi ya methali na nyimbo, semina, na elimu mashuleni, yote yakilenga kuimarisha maadili na kupunguza unyanyapaa katika jamii. Walipoulizwa kuhusu njia wanazopendekeza za kutumia Kiswahili kupinga LGBTQ miongoni mwa vijana, washiriki walitoa mapendekezo yafuatayo kama ilivyo katika Jed. 8. Programu za redio na televisheni (80), Vitabu/nyimbo za Kiswahili (50), Semina na warsha (40), na methali mpya (30). Matokeo yanaonesha kuwa njia maarufu zaidi iliyopendekezwa na washiriki ni matumizi ya programu za redio na televisheni (40%). Hii inaonesha kuwa vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kufanikisha kampeni za kuhamasisha vijana kuhusu maadili. Vitabu na nyimbo za Kiswahili zilipata 25% ya mapendekezo, zikifuatiwa na semina na warsha (20%) na methali mpya (15%). Hii inaashiria umuhimu wa kutumia mbinu za kitamaduni na kisasa kwa pamoja ili kufikia vikundi mbalimbali vya jamii.

Matokeo haya yanalingana na utafiti wa Dorn na wenzake (2024) ambao ulionesha kuwa vyombo vya habari vina jukumu muhimu katika kuhamasisha na kuelimisha jamii. Aidha, lugha na maudhui yanayotokana na muktadha wa kitamaduni, kama methali, nyimbo, na warsha, vina nguvu kubwa ya kubadilisha mitazamo ya kijamii. Matokeo haya yanaonesha kuwa mchanganyiko wa mbinu za kitamaduni na kisasa, zikiongozwa na Kiswahili, unaweza kusaidia kupinga tabia zisizoendana na maadili ya kijamii huku zikidumisha mshikamano wa kijamii. Walipoulizwa jinsi Kiswahili kinaweza kuboresha mawasiliano kati ya vijana na wazazi kuhusu maadili, washiriki walitoa mapendekezo yafuatayo kama ilivyo kwenye Jed. 9.

**Jed. 9**: Mapendekezo ya Njia za Kiswahili Kuboresha Mawasiliano Kuhusu Maadili.

| Njia | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Hadithi za Kiswahili | 70 | 35.0 |
| Mafunzo ya maadili kupitia mashairi | 60 | 30.0 |
| Kiswahili mashuleni | 50 | 25.0 |
| Familia kutumia Kiswahili | 20 | 10.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Hadithi za Kiswahili (70), Mafunzo ya maadili kupitia mashairi (60), Kiswahili mashuleni (50), na Familia kutumia Kiswahili (20). Matokeo yanaonesha kuwa njia maarufu zaidi iliyopendekezwa na washiriki ni matumizi ya hadithi za Kiswahili (35%). Washiriki wengi waliona kuwa hadithi zina nafasi muhimu ya kuwasilisha maadili kwa vijana kwa njia rahisi na ya kuvutia. Mafunzo ya maadili kupitia mashairi yalipendekezwa na 30% ya washiriki, ikionesha umuhimu wa mbinu za kisanaa katika mawasiliano. Kiswahili mashuleni kilipendekezwa na 25%, likionesha umuhimu wa mfumo rasmi wa elimu, huku familia kutumia Kiswahili ikipata 10%, ikionesha hitaji la kukuza matumizi ya lugha hii nyumbani.

Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Philippopoulos (2023), ambao ulionesha kuwa hadithi na mashairi ni njia madhubuti za kufundisha maadili ya kijamii. Aidha, Onanuga (2022) alionesha kuwa shule zina jukumu kubwa katika kuimarisha matumizi ya lugha za kiasili kama Kiswahili, ambazo zinaweza kuwa msingi wa mawasiliano bora kati ya vizazi tofauti. Matokeo haya yanaonesha kuwa mchanganyiko wa hadithi, mashairi, na elimu rasmi, pamoja na juhudi za familia, unaweza kusaidia kuimarisha maadili kupitia Kiswahili. Walipoulizwa maoni mengine kuhusu mada hii, washiriki walitoa mapendekezo yafuatayo kama ilivyo kwenye Jed. 10.

**Jed. 10**: Maoni Mengine Kuhusu Kiswahili na matumizi yake dhidi ya LGBTQ.

| Maoni | Idadi ya Washiriki | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Viongozi wa kidini kutumia Kiswahili | 90 | 45.0 |
| Vikundi vya vijana na Kiswahili | 60 | 30.0 |
| Uhamasishaji kupitia vyombo vya habari | 50 | 25.0 |
| **Jumla** | **200** | **100** |

Viongozi wa kidini kutumia Kiswahili (90), Vikundi vya vijana na Kiswahili (60), na uhamasishaji kupitia vyombo vya habari (50). Matokeo yanaonesha kuwa 45% ya washiriki walipendekeza viongozi wa kidini kutumia Kiswahili kama njia ya kufikisha maadili. Hii inadhihirisha nafasi ya viongozi wa kidini kama sauti za mamlaka na ushawishi katika jamii. Vikundi vya vijana vinavyoshirikiana kwa kutumia Kiswahili vilipendekezwa na 30%, likionesha umuhimu wa majadiliano ya vijana wenyewe katika kuimarisha maadili. Aidha, 25% waliona kuwa uhamasishaji kupitia vyombo vya habari ni njia muhimu ya kufikia hadhira kubwa na kufanikisha mabadiliko ya kijamii. Matokeo haya yanathibitisha utafiti wa Carvalho na wenzake (2024), ambao ulionesha kuwa viongozi wa kidini na vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kushawishi maadili na mitazamo ya kijamii, hasa kupitia lugha za asili. Lugha ni chombo cha msingi cha kujenga mitazamo ya kijamii, na matokeo haya yanaonesha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kama chombo madhubuti cha kukuza maadili kupitia ushawishi wa viongozi wa kidini, majadiliano ya vijana, na kampeni za vyombo vya habari.

## 6. Hitimisho

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kwa ufanisi kupinga tabia za LGBTQ, hasa kupitia matumizi yake kama lugha ya mawasiliano inayofikia watu wengi. Lugha hii inatambuliwa kuwa na uwezo wa kufundisha na kuimarisha maadili ya Kiafrika kupitia methali, semi, hadithi, mashairi, na programu za vyombo vya habari. Washiriki wengi walikubaliana kuwa Kiswahili ni chombo chenye nguvu kinachoweza kufikisha ujumbe wa maadili kwa njia inayoeleweka na inayokubalika na jamii. Kutokana na matokeo ya utafiti

huu, tunapendekeza kuwa, vyombo vya habari vinapaswa kushirikiana na viongozi wa kidini, wanaharakati wa kijamii, na wasomi kuandaa programu maalum zinazotumia Kiswahili kufundisha maadili na kuhamasisha jamii kuhusu masuala yanayohusiana na LGBTQ. Programu hizi zinapaswa kupeperushwa kupitia redio na televisheni kwa lengo la kufikia hadhira kubwa, hasa vijana

## Marejeleo

Badgett, M. V. Lee, Christopher S. Carpenter, and Dario Sansone. 2021. "LGBTQ Economics." Journal of Economic Perspectives 35 (2): 141–70.

Beasy, K., Grant, R., & Emery, S. (2023). Multiple dimensions of safe space for LGBTQ students: School staff perceptions. Sex Education, 23(1), 35-48.

Butler, J. (1990). Gender trouble: Feminism and the subversion of identity. Routledge.

Carvalho, P., Caled, D., Silva, C., Batista, F., & Ribeiro, R. (2024). The expression of hate speech against Afro-descendant, Roma, and LGBTQ+ communities in YouTube comments. Journal of Language Aggression and Conflict, 12(2), 171-206.

Chatterjee, S. S., & Mukherjee, A. (2020). Impact of COVID-19 pandemic on pre-existing mental health problems. Asian journal of psychiatry, 51, 102071.

Dorn, R., Kezar, L., Morstatter, F., & Lerman, K. (2024, October). Harmful speech detection by language models exhibits gender-queer dialect bias. In Proceedings of the 4th ACM Conference on Equity and Access in Algorithms, Mechanisms, and Optimization (pp. 1-12).

Green, A. E., Taliaferro, L. A., & Price, M. N. (2022). Understanding risk and protective factors to improve well-being and prevent suicide among LGBTQ youth. Handbook of youth suicide prevention: integrating research into practice, 177-194.

Haymer, M., Connor, S. E., Kwan, L., & Litwin, M. S. (2020, September). Modifiable health behaviors among low-income, uninsured men with prostate cancer. In Urologic Oncology: Seminars and Original Investigations (Vol. 38, No. 9, pp. 735-e1). Elsevier.

Jones, L. (2023). Language, gender and sexuality in 2022: Documenting and resisting regressive ideology. Gender & Language, 17(2).

Kaoma, K. J. (2012). Colonizing African Values. Political Research Associates.,Mthembu, S. (2023). Homosexuality is not Contemporary in South Africa: The Perceptions of Traditional and Religious Leaders towards Homosexuality. Afr. J. Gend. Soc. Dev, 12, 53-77.

Li, Y., & Fabbre, V. D. (2022). The health and well-being of LGBTQ people in mainland China: The role of social work. International social work, 65(4), 693-699.

Mayo, C. (2022). LGBTQ youth and education: Policies and practices. Teachers College Press.

Mbaru, M., Tabengwa, M., & Vance, K. (2018). Cultural discourse in Africa and the promise of human rights based on non-normative sexuality and/or gender expression: exploring the intersections, challenges and opportunities. Downloaded from the Humanities Digital Library, 177.

Oakenfull, G. W. (2024). "Genderation," Identity, and Authenticity in the LGBTQ Marketplace. Australasian Marketing Journal, 14413582241244813.

Okpokwasili, O. A. (2024). The Moral Implications of Homosexuals (LGBT). Nnadiebube Journal of Social Sciences, 4(1).

Onanuga, P. A. (2022). Navigating homophobia and reinventing the self: an analysis of Nigerian digital pro-gay discourse. Gender & Language, 16(1).

Oz, M., Yanik, A., & Batu, M. (2023). Under the shadow of culture and politics: Understanding LGBTQ social media activists' perceptions, concerns, and strategies. Social Media+ Society, 9(3), 20563051231196554.

Paiz, J. M., & Koda, K. (2021). Bringing trans, non-binary, and queer understandings to bear in language education. Critical Multilingualism Studies, 9(1), 23-45.

Philippopoulos, E. (2023). More than just pronouns–gender-neutral and inclusive language in patient education materials: suggestions for patient education librarians. Journal of the Medical Library Association: JMLA, 111(3), 734.

Ramsey, Z. S., Davidov, D. M., Levy, C. B., & Abildso, C. G. (2022). An etic view of LGBTQ healthcare: Barriers to access according to healthcare providers and researchers. Journal of Gay & Lesbian Social Services, 34(4), 502-520.

Ro, H., & Kang, J. (2025). Brand equity formation among LGBTQ+ customers: The role of brand-self identification. Journal of Brand Management, 67(1). https://doi.org/10.1177/19389655251372079.

Robinson, B. A. (2023). "They peed on my shoes": Foregrounding intersectional minority stress in understanding LGBTQ youth homelessness. Journal of LGBT Youth, 20(4), 783-799.

Rojo, M. L. (2022). Power and the role of language. Handbook of pragmatics: 25th annual installment, 107-128.

Saheed, R. O. (2023). Globalization and the emerging sexual trends in Africa. ABUAD Journal of Social and Management Sciences, 4(1), 75-91.

Schreuder, M.-C. (2021). Safe spaces, agency, and resistance: Ametasynthesis of LGBTQ language use. Journal of LGBT Youth, 18(3), 256–272.

Searle, J. R. (1995). The construction of social reality. Free Press.

Shaikh, A., Kamble, P., Daulatabad, V., Singhal, A., Madhusudhan, U., & John, N. A. (2024). Mental health

challenges within the LGBTQ community: A societal imperative. Journal of Family Medicine and Primary Care, 13(9), 3529-3535.

Smith, R. K. (2022). International human rights law. Oxford University Press.

Ugwu, N. H., Akinyemi, J. O., & Odimegwu, C. O. (2025). Sexual Practices in Africa. Second International Handbook on the Demography of Sexuality, 133-146.

Villarroya, A., & Boté-Vericad, J. J. (2023). The gender and LGBTQ perspectives in library and information science: A case study at the University of Barcelona. Library & Information Science Research, 45(2), 101238

Westwood, S. (2022). Religious-based negative attitudes towards LGBTQ people among healthcare, social care and social work students and professionals: A review of the international literature. Health & Social Care in the Community, 30(5), e1449-e1470.

Wilkins, C. L., Wellman, J. D., Toosi, N. R., Miller, C. A., Lisnek, J. A., & Martin, L. A. (2022). Is LGBT progress seen as an attack on Christians?: Examining Christian/sexual orientation zero-sum beliefs. Journal of personality and social psychology, 122(1), 73.